# <u>JUMUIYA YA ROZARI HAI ULIMWENGUNI TANZANIA</u>

NOVENA YA NOELI : 16 -24 Disemba 2021

*(Sali Novena hii kuanzia tarehe 16-24 Disemba. Novena hii ingawa inaanza kusaliwa siku moja kabla ya antifona ya Noeli, inahusiana na Antifona ya Noeli katika majina yanayotumika kumtaja Yesu kati ya tarehe 17 na 24 Disemba. Hivyo inafaa pia kusaliwa wakati familia yako inaposali Antifona ya Noeli.)*

16 DISEMBA

**Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina.**

**Sali sala ya kutubu, kasha Sali sala ya Uje Roho Mtakatifu.**

**Nia za Novena (Kila siku inawakilishwa na nia moja kati ya zote 9)**

1. Kumshukuru Mungu kwa Mema yote aliyotutendea mwaka huu 2021 na kuomba Baraka kwa mwaka ujao 2022.
2. Kuwaombea wasafiri wote msimu huu wa sikukuu wawe na safari njema.

3.Kuziombea familia zitunze uhai wa watoto wasiozaliwa bado.

4. Kuwaombea wagonjwa wote uponyaji na tuepushwe na janga la corona.

5. Kuiombea Nchi yetu ya Tanzania na viongozi wake.

6. Kuliombea Kanisa Katoliki,Baba Mtakatifu Mapadre na watawa wote wa kike na wakiume wadumu katika wito wao wakiokoa roho za watu na roho zao pia.

7. Kuombea Jumuiya ya Rozari hai Ulimwenguni kote na udumivu wa sala kwa wanachama wake.

8. Kuwaombea marehemu wote TOHARANI warehemiwe wamwone Mungu.
9. **Nia Binafsi….**

**Ant. Ya wimbo wa Enjili**

Toka mbinguni/ atakuja Mtawala na Bwana:/mkononi mwake vimo heshima na mamlaka. ***(Kwa Anayesali Asubuhi)***

Vizazi vyote/ wataniita mbarikiwa;/ kwa kuwa Mungu amemtazama mjakazi mnyonge***.( Kwa anayesali Jioni)***

SOMO FUPI; Hes. 24: 14-17

Basi sasa, tazama ninakwenda kwa watu wangu; haya, nitakuarifu mambo ambayo watu hawa watakayowatenda watu wako siku za mwisho. Akatunga mithali yake akasema, Baalamu mwana wa Beori asema yule mtu aliyefumbwa macho asema, asema, yeye asikiaye maneno ya Mungu, na kuyajua maarifa yake aliye juu, yeye aonaye maono ya mwenyezi, akianguka kifudifudi, amefumbuliwa macho.Namwona lakini si sasa, namtazama, lakini si karibu; nyota itatokea katika Yakobo, na fimbo ya enzi itainuka katika Israel; nayo itazipiga pembe za Moabu, na kuwavunjavunja wana wote wa ghasia.

SALA YA NOVENA

Ee Mchungaji mwema unayetawala Israel, uliyemuongoza Yosefu kama kondoo, uje kutulinda na kutufariji.

Baba Yetu…….Salamu Maria….Atukuzwe Baba……,

**SALA YA KUFUNGIA.**

Ee Bwana, tunakuomba usikilize kwa wema sala zetu, na kutuangazia giza la akili zetu kwa neema ya Mwanao anayekuja. Tunaomba hayo kwa njia ya Kristu Bwana wetu. Amina

Atukuzwe Baba na Mwana na Roho Mtakatifu….

**Kwa jina la baba na la Mwana na la roho Mtakatifu ,Amina.**

17 DISEMBA

**Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina.**

**Sali sala ya kutubu.**

**Weka Nia Ya Novena**

**Ant. Ya wimbo wa Enjili**

Amka,/amka, Ee Yerusalem,/fungua pingu za shingo lako, binti Sion mfungwa. **( Kwa Anayesali Asubuhi)**

Kabla/ hawajakaribiana Maria alionekana kuwa na mimba kwa Roho Mtakatifu, aleluya. **(Kwa anayesali jioni)**

SOMO FUPI Is. 11,1-2 ( Kwa anayesali Asubuhi)

Basi likatokea chipukizi katika shina la Yese, na tawi litakalotoka katika mizizi yake litazaa matunda. Na roho ya Bwana atakaa juu yake, roho ya hekima na ufahamu, roho ya shauri na uweza , roho ya maarifa na ya kumcha Bwana.

**SOMO FUPI 1 The. 5, 23 -24 ( Kwa anayesali jioni)**

Mungu wa Amani awatakase na kuwakamilisha, mpate kuhifadhiwa salama roho na mtima na mwili bila hitilafu mpaka kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristu. Yeye aliyetuita ni Mwaminifu, atimiza neno lake.

Ant. Ya Wimbo wa Enjili

**Mjue/ufalme wa Mungu u karibu;/ kweli nawaambia hautakawia ( Kwa anayesali asubui au jioni)**

**SALA YA NOVENA**

Ee Hekima, utokaye kinywani wa aliye juu kabisa, unayeujaza ulimwengu na kushikilia vitu vyote pamoja kwa nguvu na makini. Njoo utuoneshe njia ya ukweli.

Baba Yetu……Salamu Maria…..Atukuzwe Baba……..

**SALA YA KUFUNGIA**

Ee Mungu, ulitufanya sisi kuwa viumbe vipya kwa njia ya Mwanao wa pekee. Tunakuomba ulitazame kwa wema tendo hilo la huruma yako, na kutuondolea dhambi zetu zote za zamani kwa kuja kwake Mwanao. Utujalie hayo kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristu. Amina

Atukuzwe Baba na Mwana na Roho Mtakatifu….

**Kwa jina la baba na la Mwana na la roho Mtakatifu ,Amina.**

**18 DISEMBA**

**Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina.**

**Sali sala ya kutubu.**

**Weka Nia Ya Novena**

**Ant. Ya Wimbo wa Enjili**

Tulieni,/ tulieni, watu wangu, asema Bwana na Mungu wenu. **( Kwa Anayesali Asubuhi)**

Ni wewe/ utakayekuja, au tumtazamie mwingine? Mwambieni Yohane mliyoyaona: Vipofu wanaona, wafu wanafufuka, na maskini wanahubiriwa habari njema, aleluya. **( Kwa anayesali jioni)**

**SOMO FUPI Rom. 13, 11-12 ( Kwa anayesali Asubuhi)**

Isitoshe, muwe mnatambua wakati: Saa imekwisha kuwadia ya kuamka sisi katika usingizi. Kwa maana sasa wokovu wetu u karibu zaidi kuliko wakati tulipoanza kusadiki. Usiku umepungua, mchana umekaribia. Basi, tuvue matendo ya giza, na tuvae silaha za mwanga.

**SOMO FUPI Filip. 4, 4-5 ( Kwa anayesali jioni)**

Furahini daima katika Bwana. Nasema tena: Furahini. Mwenendo wenu mwema ujulikane kwa watu wote.Bwana yu karibu.

Ant. Ya Wimbo wa Enjili

**Mama Maria wa Yesu,/ alipokuwa ameposwa na Yosef, /kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.**

**SALA YA NOVENA**

Ee Adonai, Bwana Mkuu, na kiongozi wa Israel, uliyemtokea Musa katika kichaka cha moto, na kumpatia Torati mlimani Sinai, njoo kwa uwezo wako mkuu.

Baba Yetu……..Salamu Maria……Atukuzwe Baba………

**SALA YA KUFUNGIA**

Ee Mungu Mwenyezi, sisi tunaoelemewa na nira ya dhambi ya asili tunakuomba utujalie kuokolewa kwa kuzaliwa kwake Mwanao wa pekee tunayemtazamaia kuja. Tunaomba hayo kwa njia ya Kristu Bwana wetu. Amina

Atukuzwe Baba na Mwana na Roho Mtakatifu….

**Kwa jina la baba na la Mwana na la roho Mtakatifu ,Amina.**

**19 DISEMBA**

**Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina.**

**Sali sala ya kutubu.**

**Weka Nia Ya Novena**

Ant.ya wimbo wa Enjili

Amka,/ amka, vaa enzi, Ee mkono wa Bwana. **( Kwa Anayesali Asubuhi)**

Furahi/pamoja na Yerusalem,/mkashangilie ndani yake hata milele, wote mnaopenda. **( Kwa anayesali jioni)**

**SOMO FUPI Is. 2-3 ( Kwa anayesali jioni)**

Na mataifa mengi watakwenda na kusema , njooni, twende juu mlimani kwa Bwana, nyumbani kwa Mungu wa Yakobo, naye atatufundisha njia zake, nasi tutakwenda katika mapito yake; maana katika Sion itatoka sheria, na neno la Bwana katika Yerusalemu.

**SOMO FUPI Wafil. 3, 20b -21 ( Kwa anayesali jioni)**

Kutoka mbinguni anakuja Mwokozi, Bwana wetu Yesu Kristu tunayemtazamia. Naye atatengeneza mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu . Atafanya wote chini ya mamlaka yake.

Ant. Ya wimbo wa Enjili

**Naye atatangulia /mbele zake katika roho ya Eliya, ili kumwekekea Bwana watu waliotengenezwa.**

**SALA YA NOVENA**

Ewe shina la Yese, kama ishara kwa mataifa wafalme hunyamaza mbele yako, wewe ambaye mataifa yakushangilia.Njoo utuokoe, na wala usikawie.

Baba Yetu……Salamu Maria……Atukuzwe Baba…..

**SALA YA KUFUNGIA**

Ee Mungu, ulipenda kuifunulia dunia fahari ya utukufu wako Bikira mtakatifu alipojifungua.Tunakuombea utujalie tuliheshimu kwa imani yote fumbo hili kuu kujifanya mwanadamu na kulitukuza siku zote kwa unyenyekevu. Tunaomba hayo kwa njia ya Kristu Bwana wetu. Amina

Atukuzwe Baba na Mwana na Roho Mtakatifu….

**Kwa jina la baba na la Mwana na la roho Mtakatifu ,Amina.**

**20 DISEMBA**

**Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina.**

**Sali sala ya kutubu.**

**Weka Nia Ya Novena**

Ant.ya wimbo wa Enjili

Lingojewe /kama mvua Neno la Bwana/ na Mungu wetu atushukie kama umande. (**Kwa Anayesali Asubuhi)**

Huo ndio/ushuhuda alioutoa Yohane;/ Atakayekuja nyuma yangu, alikuwapo kabla yangu.**( Kwa anayesali jioni)**

**SOMO FUPI Mwa. 49, 10 (Kwa Anayesali Asubuhi)**

Fimbo ya enzi haitaondoka katika Yuda, wala mfanya sheria kati ya miguu yake, hata atakapokuja Yeye, mwenye milki, ambaye mataifa watamtii. (**Kwa Anayesali Asubuhi)**

**SOMO FUPI Eze. 34, 15 -16 ( Kwa anayesali jioni)**

Mimi mwenyewe nitawalisha kondoo zangu, nami nitawalaza, asema Bwana Mungu. Nami nitawatafuta waliopotea, nitwarudisha waliofukuzwa, nitawafunga waliovunjika, nitawatia nguvu wagonjwa; nao wanono na wenye nguvu nitwaharibui; nitwalisha hukumu.

Ant. Ya wimbo wa Enjili.

**Malaika Gabriel/alitumwa kwa mwanamwali Bikira Maria aliyekuwa ameposwa na Yosefu.**

**SALA YA NOVENA**

Ee ufunguo wa Daudi na fimbo ya Israel, unachofungua hapana awezaye kufunga tena, unachofunga hapana awezaye kufungua. Njoo uwatoe mateka gerezani, uwaangazie wale wanaokaa katika giza na katika kivuli cha mauti.

Baba Yetu……Salamu Maria…….Atukuzwe Baba………

**SALA YA KUFUNGIA**

Ee Mungu, Bikira asiye na doa alimchukua mimba Mwanao, yaani Neno wako, hapo malaika alipompasha habari. Naye Maria akawa nyumba ya Mungu na kujaa mwanga wa Roho Mtakatifu. Tunaomba utuwezeshe kuamabatana na utashi wako kwa unyenyekevu kama yeye. Tunaomba hayo kwa njia ya Kristu Bwana wetu. Amina

Atukuzwe Baba na Mwana na Roho Mtakatifu….

**Kwa jina la baba na la Mwana na la roho Mtakatifu ,Amina.**

**21 DISEMBA**

**Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina.**

**Sali sala ya kutubu.**

**Weka Nia Ya Novena**

Ant.ya wimbo wa Enjili

Msiogope /maana siku ya tano Bwana wetu atakuja. (**Kwa Anayesali Asubuhi)**

Ee Utokeaye,/ ung'aro wa mwanga wa milele na jua la haki :uje kuwaangaza wakaao gizani na kivulini mwa mauti. **( Kwa anayesali jioni)**

**SOMO FUPI Is. 7, 14b -15 (Kwa Anayesali Asubuhi)**

Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Immanuel. Siagi na asali atakula wakati ajuapo kuyakataa mabay na kuyachagua mema.

**SOMO FUPI 1 Kor. 4,5 ( Kwa anayesali jioni)**

Kwa hiyo msihukumu mapema kabla Bwana hajaja bado. Huyo atafichua yaliyofichika gizaniu, na atazifumbulisha nia za mioyo .Ndipo kila mmoja atakapopata sifa yake kwa Mungu.

Ant. Ya wimbo wa Enjili.

**Ee Mfalme wa mataifa/ na mtamaniwa wao, na jiwe la pembe, unayeunganisha yaliyoachana, uje kumwokoa mtu uliyemfanya kwa udongo.**

**SALA YA NOVENA**

Ewe jua linalochomoza, wewe ni mng'ao wa nuru ya milele na jua la haki. Njoo uwaangazie wale wakaao katika giza na katika kivuli cha mauti .

Baba Yetu……Salam Maria……Atukuzwe Baba

**SALA YA KUFUNGIA**

Ee Mungu Mwenyezi wa milele, umependa kuzaliwa kwake Mwanao kuwe shina na utimilifu wa dini yetu. Twakuomba utuweke miongoni mwa warithi wake yeye peke yake wokovu wa wanadamu wote. Tunaomba hayo kwa njia ya Kristu Bwana wetu. Amina

Atukuzwe Baba na Mwana na Roho Mtakatifu….

**Kwa jina la baba na la Mwana na la roho Mtakatifu ,Amina.**

**22 DISEMBA**

**Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina.**

**Sali sala ya kutubu.**

**Weka Nia Ya Novena**

Ant. Ya wimbo wa Enjili

Yosef, mwana wa Daudi,/Usihofu kumchukua Maria Mkeo,/maana mimba yake ni kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, aleluya. (**Kwa Anayesali Asubuhi)**

Nyesheni,/enyi mbingu juu na mawingu yamimine mwenye haki;/ nchi ifunguke na kumwotesha Mkombozi. **( Kwa anayesali jioni)**

**SOMO FUPI Is. 45, 8**

Dondokeni, enyi mbingu toka juu, mawingu na yamwage mwenye haki. Nchi na ifunuke, ili kutoa wokovu, nayo itoe haki ikamee pamoja; mimi Bwana, nimeiumba. **( Kwa anayesali Asubuhi)**

**SOMO FUPI Yak. 5, 7-8.9b . ( Kwa anayesali jioni)**

Haya, Ndugu, subirini mpaka Bwana atakapokuja, Hata mkulima anangojea mazao mazuri ya dunia. Anangojea kwa subira mvua ya vuli na masika. Nanyi subirini na kuimarisha mioyo yenu, kwani ujio wa Bwana umekaribia .Tazameni, hakimu amesimama mbele ya mlango.

Ant. Ya wimbo wa Enjili.

**Sauti ya kuamkia kwako/ilipoingia masikioni mwangu, kitoto kichanga kikaruka kwa shangwe ndani ya tumbo langu, aleluya.**

**SALA YA NOVENA**

Ewe mfalme ambaye wote wakutamani, wewe ni jiwe kuu la pembeni ambalo lawaunganisha wote .Njoo umwokoe mwanadamu ambaye ulimwumba kwa udongo.

Baba Yetu……..Salam Maria……Atukuzwe Baba…….

**SALA YA KUFUNGIA**

Ee Mungu. Ulimwona mwanadamu ameanguka katika mauti, ukapenda kumkomboa kwa kuja kwake Mwanao wa pekee. Tunakuomba utujalie sisi tunaokiri kwa unyenyekevu kwamba yeye amejifanya mwanadamu, tustahihi kushiriki ukombozi wake. Tunaomba hayo kwa njia ya Kristu Bwana wetu. Amina

Atukuzwe Baba na Mwana na Roho Mtakatifu….

**Kwa jina la baba na la Mwana na la roho Mtakatifu ,Amina.**

**23 DISEMBA**

**Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina.**

**Sali sala ya kutubu.**

**Weka Nia Ya Novena**

**Ant. Ya wimbo wa Enjili.**

Tazama,/ yote yametimia yaliyosemwa na Malaika juu ya Bikira Maria. **( Kwa anayesali Asubuhi)**

Ee Emmanuel,/ Mfalme wa Mtunga sheria wetu, matumain  ya mataifa na mkombozi wao: uje kutuokoa, Bwana Mungu wetu. **( Kwa anayesali jioni)**

**SOMO FUPI   Yak. Yer. 30, 21. 22  ( Kwa anayesali Asubuhi)**

Na mkuu wao atakuwa mtu wa kwao wenyewe, naye  mwenye kutawala atakuwa mtu wa jamaa yao; name nitamkaribisha, naye atanikaribisha maana ni nani aliye na moyo wa kuthubutu kunikaribia?Asema Bwana. Nanyi mtakuwa watu wangu, name nitakuwa Mungu wenu.

**SOMO FUPI    2 Petr 3, 8b-9  ( Kwa anayesali jioni)**

Lakini, ndugu wapenzi, msipitwe katika jambo hili: Siku moja kwa Bwana ni kama miaka elfu, na miaka elfu ni kama siku moja.Bwana hakawishi ahadi kama baadhi ya watu wanavyoudhania ukawio, lakini anawasubiria ninyi kwa sababu hapendi wengine wenu wapotee, bali wote waje kutubu.

Ant. Ya wimbo wa Enjili.

**Atakapokuja,/ Mwana wa Adamu, je, ataikuta imani duniani?**

**SALA YA NOVENA**

Ee Immanuel, wewe ni mfalme, hakimu na Mwokozi wetu, yule ambaye watu wanamgonjea . Njoo utuokoe, Bwana Mungu wetu.

Baba Yetu……Salamu Maria ……Atukuzwe Baba…….

**SALA YA KUFUNGIA**

Ee Mungu mwenyezi wa milele, tunafahamu kwamba sikukuu ya kuzaliwa kwake Mwanao inakaribia. Kwa hiyo sisi watumishi wako wakosefu tunaomba neno  wako aliyependa kuwa mwanadamu, akazaliwa na Bikirw Maria na kukaa kwetu, atujalie huruma yako. Tunaomba hayo kwa njia ya Kristu Bwana wetu. Amina

Atukuzwe Baba na Mwana na Roho Mtakatifu….

**Kwa jina la baba na la Mwana na la roho Mtakatifu ,Amina.**

**24 DISEMBA**

**Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina.**

**Sali sala ya kutubu.**

**Weka Nia Ya Novena**

Ant. Ya wimbo wa Enjili.

Leo mjue/ ya kwamba Bwana atakuja; /na kesho mtauona utukufu wake. **( Kwa anayesali Asubuhi)**

Ee Bwana, /uwape tuzo wakutumainio, / ili manabii wako waonekane waaminifu. **( Kwa anayesali jioni)**

**SOMO FUPI Isa. 11, 1-3a ( Kwa anayesali Asubuhi)**

Basi litatoka chipukizi katika shina la Yese, na tawi litakalotoka katika mizizi yake itazaa matunda. Na roho ya Bwana atakaa juu yake, roho ya hekima na ufahamu, roho Ya shauri na uweza, roho ya maarifa na ya kumcha Bwana.

**SOMO FUPI Is. 4:3 ( Kwa anayesali Alasiri / jioni)**

Tena itakuwa ya kwamba yeye aliyebaki katika sion, na yeye aliyeachwa ndani ya Yerusalemu ataitwa mtakatifu; yaani, kila mmoja aliyeandikwa miongoni mwa hao walio hai ndani ya Yerusalemu.

Ant. Ya wimbo wa Enjili

**Siku zake/ Maria zilitimia, za kumzaa Mwana mzaliwa wake wa kwanza**.

**SALA YA NOVENA**

Ewe uketiye juu ya makerubi, Mungu wa majeshi, utuangazie uso wako, nasi tutaokoka.

Baba Yetu….. Salamu Maria……….Atukuzwe Baba……

**SALA YA KUFUNGIA**

Ee Bwana Yesu, tunakuomba uje hima wala usikawie, ili kuja kwako kutufariji sisi tunaoutumainia wemawako. Unayeishi na kutawala na Mungu Baba katika Umoja wa Roho Mtakatifu, Mungu, daima na milele. Amina

Atukuzwe Baba na Mwana na Roho Mtakatifu….

**Kwa jina la baba na la Mwana na la roho Mtakatifu ,Amina.**

***<u>NOVENA HII IMEANDALIWA KUTOKA BREVIARIO YA KIMONAKI NA KITABU CHA NOVENA MBALIMBALI CHA EMILIA MKUBULO</u>***

***<u>Nawatakia Kheri ya Noeli na Mwaka mpya 2022 wenye Furaha na Baraka tele. Wenu niliye Mdudu.</u>***

***F. Masaka***

***AVE MARIA! MAPENDO NI YA MILELE……***

***********************************************************************************